JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA
TASAC

TANGAZO LA AJIRA ZA MUDA

WAINGIZA KADHIA ZA FORODHA (DATA ENTRY CLERKS)

Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) linatangaza nafasi za ajira za muda (Intern Data Entry Clerks).

Sifa za mwombaji

1. Awe Mtanzania mwenye umri usiopungua miaka kumi na nane (18) ;
2. Awe na cheti cha kumaliza kidato cha nne ;
3. Awe na uzoefu wa kutumia kompyuta;
4. Awe na ujuzi na uzoefu usiopungua mwaka mmoja wa kutumia mfumo wa forodha (TANCIS) kwa kuingiza kadhia ya ugomboaji shehena;
5. Awe na uwezo wa kujaza kadhia za forodha (TANSAD) 25 ndani ya saa nane kwa siku;
6. Awe na ujuzi na uzoefu wa kuzitambua nyaraka mbalimbali kwa ajili ya kuingiza na kutoa shehena;
7. Awe mwadilifu;
8. Wasifu (CV iliyosainiwa na mwombaji na kuainisha wadhamini wawili (Referees); na
9. Juu ya Bahasha iandikwe MAOMBI YA KAZI YA MUDA **(Intern Data Entry Clerks).**

Maombi yaandikwe kwa mkono, wasifu wa mwombaji (CV) na nakala ya vyeti, vitumwe ofisi ya Mkurugenzi Mkuu, Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), S.L.P. 989, Dar es Salaam iliyoko katika jengo la PPF Tower.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **3 Machi 2020.**

Barua zote zitapokelewa mapokezi ghorofa ya saba (Wing 701) kati ya saa nne (4) asubuhi mpaka saa tisa (9) mchana.

Limetolewa na;

Mkurugenzi Mkuu
Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC)